



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

Muongozo wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Katika Utoaji wa Huduma za Kifua Kikuu (TB) na Ukoma

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma,
Mji wa Serikali, Mtaa wa Afya
S.L.P 743, 40478 Dodoma, Tanzania

Machi, 2022

Yaliyomo

Yaliyomo	i
Vifupisho	ii
Shukrani	iii
Utangulizi	iv
SURA YA KWANZA	
Taarifa za Msingi Kuhusu Kifua Kikuu (TB) Na Ukoma.....	1
1.1 Kifua Kikuu.....	1
1.2 Kifua Kikuu Sugu	3
1.3 Ukoma	4
1.4 Kifua Kikuu Katika Makundi Maalum	6
1.5 Vikwazo vya kijinsia na haki za binadamu katika upatikanaji wa huduma za kifua kikuu na ukoma	10
SURA YA PILI	
Ugunduzi, Matibabu na Njia Za Kujikinga Dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma.	11
2.1 Ugunduzi wa Kifua Kikuu	11
2.2 Ukusanyaji, Uandaaji na Uwasilishaji wa Sampuli za Makohozi....	13
2.3 Matibabu ya Kifua Kikuu na Ukoma	19
SURA YA TATU	
Utekelezaji wa Hatua za Udhibiti wa Kifua Kikuu, Ukoma Na Magonjwa Mseto Katika Ngazi ya Jamii.	28
3.1 Utangulizi.....	28
3.2 Kazi za Udhibiti wa Kifua Kikuu, Ukoma na Magonjwa Mseto ya Kifua Kikuu Katika Jamii.....	29
SURA YA NNE	
Ufuatiliaji Natathimini ya Utekelezaji Wa Shughuli za Kifua Kikuu Na Ukoma Ngazi ya Jamii.....	39
4.1 Ufuatiliaji na Tathimini.....	39
4.2 Mchakato wa Ufuatiliaji na Tathimini.....	40
4.3 Nyenzo za Usimamizi.....	45
MAREJEO	50
VIAMBATISHO	51

Vifupisho

AZAKI	Asasi za Kiraia
CHW	Mtoa Huduma za Afya Ngazi ya Jamii
DOT	Uangalizi wakati wa kumeza dawa za TB
DR	Kifua kikuu sugu
EANNASO	Eastern Africa National Networks of AIDS and Health Service Organisations
ENGAGE TB	Mradi wa SHIRIKI UDHIBITI WA TB
LEP	Ukoma
MKUTA	Mwitikio wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukimwi Tanzania
NTP	Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma
OR- TAMISEMI	Ofisi ya Rais tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PPM	Public-Private – Mix
RCH	Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto
TB	Kifua Kikuu
TTCN	Tanzania TB Community Network
UDOM	Chuo Kikuu Cha Dodoma
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UVIKO-19	Ugonjwa wa Virusi Vya Korona uligunduliwa mwaka 2019
VVU	Virusi vya UKIMWI
WAVIU	Wanaishi na Virusi Vya UKIMWI
WHO	Shirika la Afya Duniani
XDR	Kifua Kikuu Sugu zaidi

Shukrani

Rasimu ya Mwongozo wa Watoa Huduma za Afya Ngazi ya Jamii Katika Utoaji wa Huduma za Kifua Kikuu (TB) na Ukoma umefanyiwa mapitio na kutengeneza toleo hili la pili kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Wizara ya Afya, inapenda kuwashukuru wote ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki kutengeneza toleo hili la pili la kitabu hiki. Awali shukrani kwa OR- TAMISEMI, Ndg. Pamela Kisoka na Dkt. Mageda Kihulya pamoja na waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma katika ngazi za Mikoa na Halmashauri. Pia kwa Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma, Dkt. Liberate Mleoh pamoja na Dkt. John Msaki na Dkt. Deus Kamara kwa kusimamia na kuratibu maandalizi ya kuhuisha mwongozo huu. Wizara inapenda kutoa shukran za dhati kwa wadau na Asasi za Kijamii ikiwemo Family welfare Foundation (Ndg. Jaka Mwambi), Amref Health Africa (Ndg. Lilian Ishengoma, Dkt. Rose Olotu), EANNASO/ TTCN (Ndg. Rodrick Mugishagwe), na MUKIKUTE (Ndg. Martin Kalowela) kwa mchango wao uliowezesha kukamilika kwa mwongozo huu.

Wizara pia inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mtaalam Mshauri (Consultant), Dkt. Golden Masika wa Chuo kikuu cha Dodoma kwa ushauri na mwongozo wa kitaalam katika kipindi chote cha mapitio ya mwongozo huu.

Kipekee Wizara inapenda kuwashukuru shirika la Amref Health Africa kupitia mfuko wa Dunia wa kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund ATM) kwa kuwezesha zoezi hili.

Dkt. Beatrice Mutayoba
Mkurugenzi wa Kinga

Utangulizi

Kifua kikuu (TB) ni janga la kidunia. Karibu theluthi moja ya watu duniani wanakadiriwa kuwa na maambukizi ya vimelea vya TB na wapo katika uwezekano wa kuugua TB. Tanzania ni moja kati ya nchi 30 zenye wagonjwa wengi kulingana na takwimu za Shirika la Afya Duniani.

Katika kutokomeza Kifua Kikuu nchini, Wizara ya Afya, inatekeleza mkakati wa kupambana na TB unaolenga masuala ya kijinsia, usawa na upatikanaji wa huduma bora hasa kwa wale walio katika uwezekano mkubwa wa kuugua TB na Ukoma.

Ili kufikia lengo hili, Wizara imejipanga kuongeza uibuaji wa mapema wa wagonjwa wa TB na Ukoma na kuwatibu kwa ufasaha kwa kuzingatia misingi ya upatikanaji wa huduma bora ikiwemo “ushirikishwaji wa jamii, Asasi za kijamii, pamoja na watoa huduma za Afya katika sekta za umma na binafsi”.

Hali kadhalika, mkakati huu unalenga kuongeza huduma shirikishi na jumuiishi za TB, Ukoma, UKIMWI, UVIKO-19, Kisukari, huduma za kudhibiti usugu wa dawa za TB na magonjwa mengine, pia ushirikiano wa sekta za kijamii na za binafsi katika udhibiti wa TB na Ukoma (PPM); pamoja na ushirikishwaji wa jamii kupitia vikundi vya waliopona TB na Ukoma. Mkakati huu unajielekeza katika kuongeza hamasa na utashi wa Asasi za kijamii kuingiza shughuli za TB na Ukoma katika mipango kazi na bajeti zao. Asasi hizi zinajumuisha taasisi mbalimbali zikiwemo: vikundi vya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyama vya wafanyakazi, mashirika ya dini na vyama vya kitaaluma.

Ni nini lengo la kitabu hiki?

Ushirikishwaji wa jamii katika huduma za TB na Ukoma umekuwa ukiwekewa mkazo na Mpango wa Taifa wa Kifua kikuu na Ukoma pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa miongo kadhaa sasa. Lengo la kitabu hiki ni kuwapatia watoa huduma za udhibiti wa TB na Ukoma ngazi ya jamii marejeo ya haraka wakati wa utoaji huduma ili kuleta utekelezaji bora na ufanisi kulingana na mwongozo wa utekelezaji wa udhibiti wa TB na Ukoma katika ngazi ya jamii.

Walengwa wa kitabu hiki.

Kitabu hiki kinawalenga watoa huduma za afya katika ngazi ya jamii ikiwa ni pamoja na: Vikundi vya waliopona TB, watoa huduma za afya ngazi ya jamii (CHW) na wanajamii kwa ujumla.

Dkt. Riziki Kisonga

Meneja Mpango

Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma

SURA YA KWANZA

Taarifa za Msingi Kuhusu Kifua Kikuu (TB) na Ukoma.


1.1 Kifua Kikuu

1.1.1 Maana ya kifua kikuu

Kifua kikuu ni ugonjwa wa kusendeka unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria visivyoonekana kwa macho ila kwa hadubini. Ugonjwa huu kwa jina la kitaalamu hujulikana kama Tuberculosis na kwa kifupi huitwa TB.

1.1.2 Kifua kikuu kinavyoenea

TB inaenea kwa njia ya hewa kutoka kwa mtu mwenye maambukizi ya TB kwenda kwa mtu mwingine. Mtu mwenye maambukizi ya TB anapokohoa au kupiga chafya hutoa vimelea hivyo, na mtu aliyekaribu yake anapovuta hewa huvuta na vimelea vya TB (bacteria)



Picha ya 1.1. Jinsi kifua kikuu kinavyoenea

1.1.3 Mambo Yanayochangia Maambukizi ya Kifua kikuu

- Kuwepo kwa mgonjwa mwenye vimelea kwenye jamii ambaye hajaanza matibabu:
- Kukatiza matibabu kwa mgonjwa wa TB hupelekea kuendelea kwa maambukizi kwenye jamii.
- Kukaa kwa muda mrefu maeneo yenye msongamano, pasipo na hewa na mgonjwa mwenye vimelea vya TB
- Kushuka kwa kinga mwilini kunakosababishwa na magonjwa mbalimbali au lishe duni

1.1.4 Makundi yaliyo katika hatari kubwa ya kuugua kifua kikuu.

Watu wanaoishi na wagonjwa wa TB

- Wazee na watoto (kinga zao huwa dhaifu)
- Watu wenye magonjwa yanayodhoofisha kinga za mwili (mfano watu wenye maambukizi ya VVU, kisukari, saratani, lishe duni)
- Wagonjwa waliowahi kuugua TB
- Watumishi wa afya
- Watu walio kwenye maeneo yenye msongamano mfano maeneo ya migodi, shule, gerezani n.k.

1.1.5 Aina za Kifua kikuu

TB imegawanyika katika aina kuu mbili:

1. TB ya mapafu: hushambulia mapafu
2. TB nje ya mapafu: hushambulia viungo vingine nje ya mapafu kama ubongo, mifupa, matezi, ngozi, moyo, mifuko ya mapafu na moyo n.k

1.1.6 Dalili za kifua kikuu.

Dalili kuu za TB ni kama zifuatazo:

1. Kukohoa wiki mbili au zaidi (kikohozi cha muda wowote kwa WAVIU)
2. Homa za mara kwa mara

- TB ya mapafu ndiyo inayoambukiza
- TB nje ya mapafu inajitokeza zaidi kwa watu ambao kinga za mwili zipo chini; mfano WAVIU, wenye kisukari, utapiamlo na Kansa.
- Watu wenye utapiamlo ndio huathirika na TB kwa idadi kubwa hapa Tanzania

ANGALIZO



3. Kutokwa na jasho jingi kuliko kawaida hasa wakati wa usiku
4. Kupungua uzito
5. Kutoa makohozi yaliyochanganyika na damu

Wagonjwa hawa wanatakiwa kuchunguzwa makohozi ili kubaini vimelea vya TB. Aidha kwa wagonjwa wa TB nje ya mapafu wanaweza kuwa na dalili nyingine kama kuvimba tezi, kujaa tumbo nk, kulingana na sehemu iliyoshambuliwa.

1.2 Kifua Kikuu Sugu

1.2.1 Maana ya kifua kikuu sugu

Hutokea pale ambapo dawa mbili (2) za **Rifampicin na Isoniazid** kati ya nne (4) zinazotumika kutibu TB ya kawaida kushindwa kufanya kazi kutokana na usugu wa vimelea vya TB

1.2.2 Kifua Kikuu Sugu zaidi (XDR)

Hutokea wakati mgonjwa mwenye TB sugu anapopata usugu wa dawa zinazotumika kutibu TB sugu kwa daraja la pili. TB sugu husambaa kwa kupitia hewa kutoka kwa mtu mwenye maambukizo ya TB sugu wakati anapokohoa, kuongea au kupiga chafya

- Dalili za TB sugu zinafanana na dalili za TB ya kawaida. Mgonjwa mwenye sifa tajwa hapo juu anaweza kuwa na TB sugu. Hivyo toa rufaa mapema kwa uchunguzi.

KUMBUKA



1.2.3 Visababishi vya Kifua Kikuu Sugu

Maambukizo kutoka kwa mgonjwa wa TB sugu. Matumizi holela ya dawa za TB (bila kufuata ushauri wa watoa huduma)



Watu wenye viashiria vifuatavyo wanaweza kuwa na TB sugu

- Ametibiwa TB bila kupona.
- Amesitisha matibabu ya TB.
- Amewahi kuumwa TB mara mbili au zaidi na kutibiwa bila kupona.
- Anaishi karibu na mgonjwa aliyegundulika kuwa na TB sugu.

1.3 Ukoma

1.3.1 Maana ya Ukoma

Ukoma (leprosy) ni ugonjwa wa kuambukiza wa kusendeka unaosababishwa na bakteria ambao hushambulia mishipa ya fahamu pamoja na ngozi. Ugonjwa wa ukoma huambukiza kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa pale anapopumua au kupiga chafya. Baada ya maambukizi mgonjwa anaweza kukaa kwa kipindi kati ya miaka 3 mpaka 20 pasipo kuonyesha dalili zozote.

1.3.2 Mambo Yanayochangia Kuenea Kwa Ukoma

- Kuwepo kwa mgonjwa mwenye vimelea kwenye jamii ambaye hajaanza matibabu.
- Kukaa kwa muda mrefu maeneo yenye msongamano, pasipo na hewa na mgonjwa mwenye vimelea vya ukoma.

1.3.3 Aina za Ukoma

Kuna aina kuu mbili za Ukoma

1. **Ukoma hafifu (PB):** huu ni ukoma wenye vimelea vichache na mabaka yake ni chini ya matano.
2. **Ukoma mkali (MB):** huu ni ukoma wenye vimelea vingi na mgonjwa anakuwa na mabaka zaidi ya matano, na dalili nyingine zote za ukoma.

Mgonjwa huyu anauwezo wa kuambukiza watu wengine pale anapopumua au kupiga chafya kama hajaanza matibabu

1.3.4 Dalili za Ukoma

Baka au mabaka ya rangi ya shaba yasiyouma wala kuwasha au kukosa hisia sehemu yeyote ya mwili.




Baka

Mabaka

Picha no 1.2. Dalili za mabaka kwa wagonjwa wa ukoma.

Kuvimba au kuuma kwa mishipa ya fahamu ya mikono, miguu, uso na wakati mwingine, mishipa mikubwa ya shingo



Mishipa ya fahamu iliyovimba

Picha no 1.3. Dalili za kuvimba mishipa ya fahamu kwa wagonjwa wa ukoma.

- Unapopata mgonjwa mwenye mojawapo ya dalili kati ya mabaka yasiyo na hisia, kuvimba kwa mishipa ya fahamu na vidonda visivyopona mpe rufaa mgonjwa wako kwenda kituo cha tiba kilicho karibu. Fanya uchunguzi kwa watu waliopo kwenye familia yake pia.

Kuwepo kwa ganzi mikononi, miguuni au sehemu nyingine za mwili. Kutokwa na vinundu sehemu ya masikio, pua na nyinginezo ambazo zina ganzi.



Vinundu kwenye masikio

KUMBUKA



Picha no 1.4. Dalili za vinundu kwenye masikio kwa wagonjwa wa ukoma.

Kuwepo kwa vidonda visivyouma. Kupata ulemavu wa viungo



Picha no 1.5. Dalili za ulemavu wa viungo kwa wagonjwa wa ukoma.

1.4 Kifua Kikuu Katika Makundi Maalum

1.4.1 Kifua Kikuu kwa Watoto

Kifua kuu (TB) ni kati ya magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha vifo kwa watoto duniani. Dalili za TB kwa watoto zinafanana na dalili za magonjwa mengine kama utapiamlo na VVU hivyo kusababisha ugumu katika kugundua ugonjwa huo. Hivyo, unapo dalili kati ya zilizoonyeshwa hapo chini unapaswa kuchukua hatua ya kutoa rufaa au kumsindikiza mgonjwa kituo cha kutolea huduma za afya.

1.4.2 Dalili za Kifua Kikuu kwa Watoto



Kukohoa wiki 2 au zaidi kwa (kikohozi cha muda mrefu)



Kikohozi cha muda wowote (kwa mtoto mwenye kuishi na VVU)



Kutoongezeka uzito au kupungua uzito
(kadi ya kliniki ya mtoto)



Homa za mara kwa mara, bila sababu ya msingi



Kupungua kwa uchangamfu au kucheza na kuwa hana raha kama kawaida yake



Kupumua kwa shida

1.4.3 Maambukizo Mseto ya TB na VVU

Maambukizo ya VVU yamesababisha ongezeko la wagonjwa wa TB duniani hasa katika ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania. UKIMWI ni kifupisho cha maneno: Upungufu wa Kinga Mwilini hutokea baada ya VVU kushambulia kinga ya mwili kusababisha dalili mseto za maradhi mbalimbali yakiwemo magonjwa nyemelezi kama TB

Mahusiano ya Kifua Kikuu na VVU

1. Mtu anaweza kuishi na vimelea vya TB bila kuugua TB
2. Kinga ya mwili inaposhuka husababisha kupata magonjwa nyemelezi ikiwemo TB, hivyo kuchangia kasi ya kuongezeka kwa ugonjwa wa TB
3. TB ni ugonjwa unaoongoza miongoni mwa magonjwa nyemelezi kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na huchangia hadi asilimia 30 ya vifo
4. TB hujitokeza endapo kinga ya mwili itapungua kutokana na sababu mbali mbali.
5. VVU ni sababu kubwa ya kupungua kwa kinga mwilini na kusababisha magonjwa nyemelezi kama TB
6. UKIMWI unaongeza uwezakano wa TB kurudia mara kwa mara na unachangia kwa sehemu kubwa kupata TB nje ya mapafu
7. UKIMWI unaongeza kasi na makali ya TB na hivyo hivyo TB inaongeza kasi na makali ya UKIMWI

Mahusiano haya ya TB na VVU yameleta changamoto na kurudisha nyuma mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa TB.

1.4.4 Kifua Kikuu na Kisukari

Ugonjwa wa kisukari ni miongoni mwa magonjwa yanayopungua kinga za mwili, hivyo kusababisha mgonjwa kuugua TB kwa urahisi.

Mahusiano ya TB na Kisukari

Kisukari ni kichocheo cha kusababisha mtu mwenye maambukizi ya TB kuugua ugonjwa wa TB. Kisukari ni kihatarishi cha kurudiwa na ugonjwa wa TB. TB inaweza kuongeza kasi ya mtu mwenye vidokezo vya sukari kuugua kisukari. TB inaweza ikazuia sukari kurudi katika kiwango chake cha kawaida.

- Dalili za TB kwa mgonjwa wa kisukari ni sawa na dalili za TB kwa mgonjwa wa kawaida. Mchunguze mgonjwa wa kisukari na kutoa rufaa kama ana dalili za TB.

KUMBUKA



1.4.5 Kifua Kikuu na UVIKO-19 (COVID-19)

Ugonjwa wa Virusi vya Korona unafanana na homa ya mafua inayoambukizwa kwa kasi. UVIKO-19 ni kifupisho cha Ugonjwa wa Virusi vya Korona vilivyogunduliwa mwaka 2019. Kwa Kiingereza, UVIKO ni COVID (Corona Virus Disease). Katika kifupisho UVIKO-19, 'U' kinawakilisha 'Ugonjwa,' 'VI' 'Virusi,' na 'KO' ni Korona.

Dalili za kawaida za UVIKO-19.

1. homa,
2. uchovu
3. kikohozi kikavu.
4. Kupiga chafya
5. kupumua kwa shida
6. Kupoteza hamu na au ladha ya chakula
7. Baadhi ya wagonjwa wanaweza kuwa na maumivu makali ya mwili,
8. kutokwa kamasi,
9. vidonda kooni
10. kuhara.

Mara nyingi dalili hizi huwa si kali na huanza polepole. Watu wengine huambukizwa lakini hawaonyeshi dalili zozote na huwa hawajisikii vibaya. Watu wengi (takribani asilimia 80) huona kutokana na ugonjwa huu bila kuhitaji matibabu maalum. Watu huambukizwa UVIKO-19 wanapogusa vitu au sehemu yenye virusi na kujigusa machoni, puani au mdomoni. Wakati mwingine ugonjwa huu unaweza kusambaa kutoka mtu mmoja kwenda mtu mwingine kupitia vitonetone wakati mtu aliyeambukizwa anapopiga chafya, anapokohoa au anapopumua.

Athari za UVIKO-19 kwa Huduma za TB na Ukoma

Kupungua kwa mahudhurio ya wateja katika vituo va kutolea huduma za afya. Kubadilika kwa ratiba za uendeshaji wa kliniki za TB na ukoma na magonjwa mengine. Kupungua kwa huduma za afya majumbani na huduma mkoba. Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za TB na ukoma kubadilishwa matumizi kwa muda na kutoa huduma za UVIKO-19.

Mambo ya Kuzingatia ili Kuendeleza Huduma za TB na Ukoma Kwenye Jamii.

CHW wanapaswa kuendelea kutoa huduma za TB na ukoma kwa jamii kwa kufuata miongozo iliyopo ya kujikinga na UVIKO-19.

1.4.6 Kifua Kikuu na Silikosisi

Silikosisi ni ugonjwa wa mapafu unaosababishwa na kuvuta hewa yenye madini ya ulanga (silika). Ugonjwa hutokea zaidi kwenye maeneo ya wachimbaji wa madini. Ugonjwa huu hutokea baada ya muda mrefu kupita toka mtu alipovuta hewa yenye mchanganyiko wa vumbi la madini ya ulanga. Watu wenye ugonjwa wa silikosisi wapo katika hatari kubwa ya kuugua TB, saratani na magonjwa mengine.

Watu walio katika hatari kubwa ya kupata silikosisi

- Wachimbaji wa madini
- Wafanyakazi wa viwanda vya chuma
- Wajenzi wa nyumba na barabara
- Wafanyakazi wa viwanda vya kutengeneza vioo
- Wapasua miamba
- Fundi wa kupaua
- Wakulima

Dalili za ugonjwa wa silikosisi

- Kikohozi kinaweza kuwa kikavu au chenye makohozi
- Maumivu ya kifua
- Kupumua kwa shida
- Mwili kuchoka
- Kupungua uzito
- Homa za vipindi
- Kuvimba kwa miguu
- Midomo kuwa ya samawati (bluu)

- Dalili za silikosisi na TB zinafanana.
- Mgonjwa wa silikosisi ana uwezekano mkubwa wakuugua TB.
- Chunguza kwa makini wagonjwa wote walio katika hatari ya kupata silikosisi. Uonapo dalili tajwa hapo juu mpe rufaa mgonjwa au chukua sampuli kwa uchunguzi.

1.4.7 Kifua Kikuu na Utapiamlo

Utapiamlo ni hali ya kuwa na lishe duni kuendana na mahitaji ya mwili. Watu wenye utapiamlo wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuambukizwa na kuugua TB tofauti na watu wasio na utapiamlo. Hapa nchini watu wenye utapiamlo ndio wanaoongoza kwa idadi kubwa ya wanaougua ugonjwa wa TB. Pia TB hupelekea mtu kuingia katika utapiamlo kwa kupoteza viini lishe.

KUMBUKA



Dalili za utapiamlo

- Chunguza dalili za TB kwa mtu mwenye utapiamlo, mpe rufaa kwenda kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi.

KUMBUKA



- Udumavu kwa watoto
- Kukonda,
- Kasi ndogo ya kufikiri na kusinziasinzia.
- Kupata magonjwa mengine kama TB kwa urahisi.
- Kuharisha mara kwa mara, na kudhoofika Zaidi

1.5 Vikwazo vya kijinsia na haki za binadamu katika upatikanaji wa huduma za kifua kikuu na ukoma

Watu wote katika jamii wana haki sawa katika kupata huduma za TB na ukoma. Vikwazo vya kijinsia ni kama vile wanawake kusubiri kupewa ruhusa na wenzi wao ili waweze kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wanapoona dalili za TB au ukoma na huduma nyinginezo. Kila mtu ana haki yakutokunyanyapaliwa anapogundulika kuwa na ugonjwa wa TB au ukoma.

- Kuchunguza vikwazo vya kijinsia na viashiria vya ukiukwaji wa haki za binadamu katika jamii na

KUMBUKA



SURA YA PILI

Ugunduzi, Matibabu na Njia Za Kujikinga Dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma.

2.1 Ugunduzi wa Kifua Kikuu

Ugunduzi wa TB ndio msingi wa utoaji wa huduma za TB. Ugunduzi unaweza kuwatambua wale wote wenye vimelea vya ugonjwa wa TB na kuwaweka kwenye matibabu ili kupunguza uwezekano wa kuendelea kueneza ugonjwa wa TB. Kuna njia mbili za ugunduzi wa TB. Njia hizo ni:

- Ugunduzi wa TB kulingana na historia ya mgonjwa
- Ugunduzi wa TB kulingana na vipimo vya maabara ambayo hutegemea sampuli za makohozi.

2.1.1 Ugunduzi wa Kifua Kikuu Kulingana na Historia ya Mgonjwa

Historia ya ugonjwa hupatikana kwa kumhoji mgonjwa kuhusu:

- Dalili za TB (kama ilivyotajwa hapo juu)
- Historia ya ugonjwa wa TB
- Kuwepo kwa magonjwa ya kusendeka kama VVU/UKIMWI, kisukari, saratani, utapiamlo n.k
- Historia ya kuishi na mgonjwa wa TB
- Uvutaji wa sigara
- Matumizi ya dawa za kulevya
- Historia ya kufanya kazi katika migodi
- Kuvimba tezi sehemu za mwili hasa shingoni.

Vipimo vya picha (X-ray) na score chart, hufanyika kumsaidia daktari kufikia maamuzi ya ugunduzi huu wa TB kwa wale wahisiwa wa TB ambao vipimo vya maabara havikuonyesha vimelea vya TB lakini bado wana dalili za TB.

2.1.2 Ugunduzi wa Ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa Njia za Maabara

Hii ndiyo njia sahihi ya uchunguzi wa TB inayopendekezwa na Mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Tanzania. Njia hii inafanyika katika vituo vya kutolea huduma za afya vyenye uwezo wa kufanya uchunguzi huo. Kuna vipimo mbalimbali vya kimaabara ambavyo vinaweza kutumika katika uchunguzi wa TB kama vile:

Ugunduzi kwa njia ya hadubini (Microscopy):

Hii ni njia ya uchunguzi wa vimelea vya TB kwenye makohozi kwa kutumia hadubini maalumu. Njia hii ya uchunguzi huhitaji sampuli mbili za makohozi (sampuli ya kwanza ni pale mhisiwa anapofika kituoni au kutembelewa na mhudumu ngazi ya jamii na sampuli ya pili hutolewa asubuhi ya siku inayofuata baada ya kuamka kabla ya mhisiwa wa TB kula chochote. Majibu ya kipimo hiki huchukua muda wa saa 24.

Ugunduzi kwa njia ya vinasaba vya vimelea wa TB (GeneXpert/TruNat):

Hii ni njia ya uchunguzi wa vimelea vya TB kwenye makohozi kwa kutumia mashine maalumu za uchunguzi wa vinasaba vya vimelea wa TB. Njia hii ni rahisi na hutumia muda mfupi kutoa majibu. Njia hii huhitaji sampuli moja tu ya makohozi.

Ugunduzi kwa kutumia panya maalumu waliofundishwa kugundua ugonjwa wa kifua kikuu:

Njia hii ilianza kutumika mwaka 2007 katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Mpaka sasa inatumika katika baadhi ya maeneo nchini (Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma). Hii ni njia mojawapo ya uchunguzi wa awali wa vimelea vya TB.

Vipimo vingine vya kimaabara.

Hivi ni pamoja na uchunguzi wa TB kwa njia ya uoteshaji wa vimelea vya TB (culture) na kupima uwezo wa dawa. Pia tafiti mbalimbali zinaendelea ili kuangalia uwezekano wa kutumia mkojo na kinyesi cha binadamu katika upimaji wa TB.

2.2 Ukusanyaji, Uandaaji na Uwasilishaji wa Sampuli za Makohozi

2.2.1 Maana ya Sampuli ya Makohozi

Sampuli ya makohozi ni utando-telezi mzito unaotolewa katika mapafu kwa kukohoa, kisha kuwekwa kwenye chombo maalum ili kupelekwa maabara kwa vipimo. Makohozi ya mtu mwenye TB huwa na machanganyiko wa vimelea vya bacteria wa TB, pamoja na seli nyeupe zinazopambana na bacteria hao.

2.2.2 Njia Salama za Ukusanyaji wa Sampuli za Makohozi

Sampuli bora ya makohozi ni muhimu kwa uchunguzi wa kimaabara wa TB. Mhisiwa wa TB anapaswa kufika katika kituo cha kutolea huduma za afya ili kutoa sampuli za makohozi na kufanyiwa uchunguzi mwingine. Ikiwa mhisiwa wa TB hawezi kufika katika kituo cha kutolea huduma za afya kwa sababu zilizo juu ya uwezo wake, basi mtoa huduma wa afya ngazi ya jamii anaweza kukusanya sampuli kutoka kwa mhisiwa huyo na kuiwasilisha. Mhisiwa anapaswa kueleweshwa kuhusu:

- Tofauti kati ya makohozi na mate
- Umuhimu wa kuvuta pumzi sana (deep breathing) wenye tija kabla ya kutoa sampuli ya makohozi.

- Ukusanyaji wa sampuli yoyote una hatari kwa mtoa huduma; mfano kumwagikiwa na sampuli ya makohozi.
- Chukua tahadhari kwa kufuata kanuni za kudhibiti maambukizi wakati wa ukusanyaji wa sampuli.

KUMBUKA



2.2.3 Hatua za Ukusanyaji wa Sampuli ya Makohozi

I. Hatua ya kwanza: Maandalizi

Andaa vifaa vya kukusanyia sampuli na vya kujikinga

Vifaa vya kukusanyia sampuli

Kikopo cha kuweka sampuli



Box dogo la kuhifadhi kikopo cha sampuli



Kalamu ya kuandika taarifa za mhisiwa



Fomu ya rufaa (TB/LEP 15) ya kujaza taarifa za mhisiwa na sampuli kwa ajili ya kwenda kwenye uchunguzi



Vifaa vya kujikinga wakati wa kuandaa na kufunga sampuli

Maji tiririka, sabuni na tishu/kitambaa cha kujikaushia kwa ajili ya kunawa kabla ya kupokea sampuli na baada ya kuiandaa na kuihifadhi kwenye boksi



Mipira ya mkononi (gloves), ya kuvaa wakati wa kupokea sampuli



Barakoa, ya kuvaa na kujikinga wakati wa kupokea sampuli na muda wote unapokuwa na mhisiwa wa TB



Tumia mipira ya mikononi mara moja tu kila unapoandaa au kushika kopo/chupa iliyobeba sampuli. Vua mipira ya mikononi kabla ya kutumia vifaa vingine kama vile simu ya mkononi n.k Pia wakati wote unaposhika kopo lenye sampuli vaa barakoa.

II. **Hatua ya Pili:** Ukusanyaji wa Sampuli

Muelekeze mhisiwa kuhusu kikopo cha kutolea sampuli. Muelekeze namna atakavyotakiwa kuweka sampuli, na sampuli bora inayotakiwa



Muombe mhisiwa kusukutua vizuri kwa maji safi na salama kama ana mabaki ya kitu kingine mdomoni kutoka



Mpatie mhisiwa kikopo cha kutolea sampuli baada ya kukiandika jina lake

Muelekeze aende nje mbali na watu wengine sehemu yenye mzunguko wa hewa ya kutosha au kama ni ndani kuwa karibu na dirisha lililo wazi mbali na watu wengine. Hii itahakikisha haambukizi watu wengine wakati wa kutoa sampuli ya kohozi.

Mwambie ajilegeze na kuvuta pumzi ndani na nje mara tatu.



Akohoe kwa nguvu ili kutoa makohozi ya ndani ya mapafu na kuweka kwenye kopo. Awe mwangalifu kuwa hakuna makohozi yanayotoka nje ya kopo



Akohoe makohozi mengi kujaza sehemu ya chini ya kopo



Makohozi yanapokuwa mengi kwenye kopo, afunike na kufunga kwa kukaza mfuniko wa kopo lenye makohozi



Endapo atashindwa kutoa makohozi, msauri aende nyumbani, na akohoe makohozi mara tu aamkapo asubuhi (makohozi hujikusanya wakati wa usiku mtu akiwa amelala)



Kuvuta mvuke kunaweza kulainisha makohozi kwenye mapafu hivyo kuleta unafuu wa wakati wa kukohoa

Arudishe kopo lenye makohozi lililofungwa vizuri kwa mtoa huduma



III. **Hatua ya Tatu:** Uhakiki wa Ubora wa Sampuli

- Hakikisha ubora wa sampuli wakati wa kupokea
- Yawe ni makohozi na si mate.
- Kwa kawaida makohozi ni mazito, yenye rangi nyeupe, njano hadi kijani.
- Sampuli zenye damu huonekana nyekundu au kahawia.
- Mate au kamasi hayafai kutumika kama sampuli.



Picha no 2.1. Ubora tofauti tofauti wa sampuli za makohozi.

Kwa maelezo ya video kuhusu uchukuaji wa sampuli za makohozi angalia kwenye anuani hii ya mtandao https://www.youtube.com/watch?v=2sd2d2_pNBA

2.2.4 **Kuandaa na Kuwasilisha Sampuli za Makohozi**

Hatua

- Hakikisha vikopo vya makohozi vimekazwa barabara na kinalandana na fomu husika ya rufaa ya sampuli ya makohozi (TB/LEP 15)
- Fungasha kikopo cha makohozi kwenye kifuko cha plastiki au chombo maalum kuzuia kusibika (contamination)
- Fungasha sampuli zote kwenye sanduku la baridi au box la kusafirishia lililowekwa lebo sawasawa

- Hakikisha sampuli zote zinapelekwa kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili uchunguzi mara moja



Picha no 2.2. Uwasilishaji wa sampuli za makohozi katika kituo cha kutolea huduma za afya.

2.2.5 Ugunduzi wa Kifua Kikuu kwa Watoto

Ugunduzi wa TB kwa watoto bado upo chini kulingana na takwimu za Mpango wa Taifa wa TB na Ukoma Tanzania. Juhudi kubwa zinatakiwa kufanywa ili kuwagundua watoto wengi zaidi wenye TB. Hata hivyo kuna changamoto kubwa ya utoaji wa makohozi kwa watoto kwa sababu watoto wengi humeza makohozi. Hivyo basi mtoto chini ya umri wa miaka mitano anapohisiwa kuwa na TB apewe rufaa kwenda kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi.

2.2.6 Ugunduzi wa Ukoma

Ugunduzi wa ukoma hufanyika katika hatua mbili kama ifuatavyo:

Uchunguzi kulingana na historia ya mgonjwa

- Amewahi kuishi na mgonjwa wa ukoma,

- Ana dalili za ukoma.

Uchunguzi wa kimaabara

- Kuchukua sampuli toka sehemu iliyoathirika na ugonjwa wa ukoma.

2.3 Matibabu ya Kifua Kikuu na Ukoma

Matibabu ya TB na ukoma ndio msingi wa udhibiti wa magojwa ya TB na ukoma katika jamii. Magonjwa ya TB na ukoma yanatibika na kupona kabisa. Mgonjwa wa TB/ukoma asipotibiwa vizuri anaweza:

- Kuambukiza watu wengine katika jamii (ambapo kwa mwaka mgonjwa wa TB anaweza kuambukiza watu 10-20)
- Kuwa na madhara mengine baadae ikiwemo ulemavu wa kudumu kwa wagonjwa wa ukoma
- Kusababisha vimelea vya TB/ukoma kupata usugu katika dawa zinazotumika kutibu magonjwa hayo.
- Kufa kutokana na ugonjwa

Dawa za kutibu TB/ukoma zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali na binafsi bila malipo yoyote.

2.3.1 Malengo ya Matibabu ya TB na Ukoma:

Matibababu ya TB na ukoma yana malengo ya:

- Kuponya ugonjwa wa TB na ukoma hivyo kurudisha ubora wa maisha na uzalishaji
- Kuzuia vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa TB na ukoma na madhara yake
- Kupunguza maambukizi kwa watu wengine
- Kuzuia usugu wa vimelea kwenye dawa

- TB na ukoma vinatibika na kupona kabisa. Dawa zake hutolewa bila malipo katika vituo vyote vya huduma za afya vya serikali na binafsi.

ANGALIZO



2.3.2 Matibabu ya Kifua Kikuu

Muda wa Matibabu ya Kifua Kikuu

Mgonjwa atapaswa kumeza dawa za TB kwa kipindi cha siku 168 (miezi sita). Matibabu hayo yamegawanyika katika vipindi viwili ambavyo ni:

- **Kipindi cha awali:** Mgonjwa atapaswa kumeza dawa za TB kwa siku 56 (miezi 2) na zitakuwa mseto wa dawa nne. Miezi miwili ya kwanza mgonjwa atakuwa anapewa dawa kila baada ya wiki moja na kurudi katika kituo kwa ajili ya muendelezo na uchunguzi wa matumizi na madhara ya dawa.
- **Matibabu ya muendelezo:** Mgonjwa atapaswa kumeza dawa kwa muda wa siku 112 (miezi 4) na zitakuwa mseto wa dawa mbili. Katika kipindi hiki mgonjwa atakuwa anapewa dawa kila baada ya wiki mbili au kama vile itakavyoelekezwa na mtoa huduma, ili mgonjwa kila mara awe anafanyiwa uchunguzi wa matumizi na madhara ya dawa.

Uchaguzi wa Mahali pa tiba na Msimamizi kwa Matakwa ya Mgonjwa (PCT)

Huu ni utaratibu wa kumpa mgonjwa wa TB uhuru wa kuchagua mahali pa matibabu ya kila siku na mtu atakayemsimamia. Mgonjwa atachagua kumeza dawa kila siku katika kituo cha huduma za afya na kusimamiwa na mhudumu wa afya au nyumbani chini ya usimamizi wa mtu aliyemchagua. Iwapo atachagua kumeza nyumbani, msimamizi wa dawa za TB anatakiwa kuhakikisha mgonjwa anameza dawa kama inavyoshauriwa. Aidha ataweka kumbukumbu ya umezaji wa dawa za kila siku na kuambatana na mgonjwa kwenda kwenye kituo cha huduma za afya kuchukua dawa au pale itakapohitajika.

Uangalizi Wakati wa Kumeza Dawa za Kifua Kikuu (DOT)

DOT ni utaratibu wa umezaji wa dawa za TB chini ya uangalizi wa mtoa huduma za afya au mtu aliyechaguliwa na mgonjwa kumsimamia katika kipindi chake cha matibabu. DOT ni msingi wa tiba ya TB ambapo husaidia kuhakikisha usahihi wa vidonge, idadi ya vidonge na muda muafaka wa umezaji dawa kwa kipindi chote cha matibabu kama inavyoelekezwa. Hii ni muhimu ili kumponyesha mgonjwa, kuzuia usugu wa dawa na kuepuka TB kuenea kwa watu wengine katika jamii. DOT hufanyika:

- Kituo cha huduma za afya—ambapo mgonjwa wa TB hufika katika kituo kila siku ili kumeza dawa chini ya uangalizi wa mtoa huduma
- Nyumbani—ambapo msimamizi aliyechaguliwa na mgonjwa humsimamia mgonjwa katika umezaji dawa. Msimamizi huambatana na mgonjwa wa TB kwenda katika kituo cha huduma za afya kuchukua dawa kila wiki katika matibabu ya mwanzo na kila baada ya wiki mbili wakati wa matibabu ya muendelezo.

- Mgonjwa atatakiwa kumeza dawa kituoni chini ya uangalizi wa mtoa huduma za afya pale anapoanzishiwa matibabu ya TB.
- Kama amechagua kumeza dawa chini ya uangalizi nyumbani, mgonjwa atapewa dawa na kuondoka nazo kwa ajili ya umezaji chini ya usimamizi nyumbani.

KUMBUKA



Athari Zinazoweza Kutokana na Matumizi ya Dawa za Kifua Kikuu

Wagonjwa walio wengi wa TB humaliza matibabu bila kupata athari zozote za dawa. Kila mgonjwa wa TB anatakiwa kuelimishwa juu ya athari zinazoweza kujitokeza wakati wa umezaji dawa za TB. Maelezo yatolewe juu ya athari ndogo ndogo na kubwa ambazo mgonjwa anaweza kuzipata. Wagonjwa wanaopata athari ndogondogo wanatakiwa kuendelea na matibabu na wagonjwa wanaopata athari kubwa wapewe rufaa kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi zaidi na matibabu.

Kwa kila athari za dawa, mtoa huduma za afya ngazi ya jamii atapaswa kuchukua hatua kama ifuatavyo.

Athari ndogo ndogo	Hatua za kuchukua
<ul style="list-style-type: none"> Kichefuchefu, kukosa hamu ya kula, maumivu ya tumbo, gesi 	<ul style="list-style-type: none"> Mshauri aendelee na matibabu
<ul style="list-style-type: none"> Uchovu wa mwili 	<ul style="list-style-type: none"> Mtoe hofu na mshauri mgonjwa aendelee na dawa pamoja na chakula au kinywaji (juisi, maji)
<ul style="list-style-type: none"> Mapigo ya moyo kwenda mbio 	<ul style="list-style-type: none"> Mshauri aendelee na matibabu na kunywa maji mengi
<ul style="list-style-type: none"> Mkojo wa manjano/ mwekundu 	<ul style="list-style-type: none"> Mhakikishie mgonjwa kuwa hali hiyo ni ya kawaida na anatakiwa kunywa maji mengi na kuendelea na matibabu
<ul style="list-style-type: none"> Maumivu ya viungo 	<ul style="list-style-type: none"> Mshauri mgonjwa aende kwenye kituo cha kutolea huduma za afya
<ul style="list-style-type: none"> Miguu kuwaka moto 	<ul style="list-style-type: none"> Mshauri mgonjwa aende kwenye kituo cha kutolea huduma za afya

Athari kubwa	
<ul style="list-style-type: none"> Harara na muwasho wa ngozi Ngozi na/au macho kuwa ya njano Kutapika mara kwa mara Kutosikia Kizunguzungu Matatizo ya kuona 	<p>Mshauri asimamishe matibabu na mhimize kwenda kituo cha tiba haraka</p>

2.3.3 Dawa za Kifua Kikuu Wakati wa Ujauzito au Kunyonyesha

Mama mjamzito mwenye TB anaweza kumuambukiza mtoto wake ugonjwa wa TB wakati wa ujauzito na kunyonyesha akishajifungua. Hivyo ni muhimu kwa mama mjamzito au anayenyonyesha mwenye TB kutumia dawa kwa usahihi ili kuzuia maambukizi kwenda kwa mtoto.

Wakati wa Ujauzito

Dawa za TB ni salama wakati wa ujauzito. Dawa za TB hutolewa kwa wagonjwa wenye TB na TB sugu. Kuna baadhi ya dawa za TB hasa TB sugu hazitakiwi kutumiwa na mjamzito. Hivyo kabla ya kuanza dawa ni muhimu kuonana na mtaalamu wa afya kwa uchunguzi na kuchagua tiba sahihi kwake.

Wakati wa Kunyonyesha

Dawa za TB ni salama katika kipindi cha kunyonyesha, hivyo mama anayenyonyesha anatakiwa kutumia ili pia kumkinga mwanaye na ugonjwa wa TB. Kuna baadhi ya dawa za TB sugu hazitakiwi kutolewa kwa mama anayenyonyesha.

- Wanawake wanaotumia vidonge vya uzazi wa mpango wanapogundulika kuwa na TB, wanatakiwa kuchagua njia mbadala za uzazi wa mpango kwa kuwa dawa za TB zinadhoofisha utendaji kazi wa vidonge vya uzazi wa mpango.

ANGALIZO



2.3.4 Matibabu ya Kifua Kikuu kwa Watoto

Matibabu ya TB kwa watoto hayana tofauti sana na yale ya watu wazima. Watoto hupata dawa mseto ulio katika makundi mawili:

- Kundi la kwanza ni mseto wa dawa tatu – hutolewa kwa kipindi cha awali cha matibabu (miezi 2-siku 56)
- Kundi la pili ni dawa mbili - Hutolewa kipindi cha muendelezo cha matibabu (miezi 4 – siku 112)

2.3.5 Matibabu ya Kifua Kikuu kwa Watu Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (WAVIU)

Matibabu ya TB kwa WAVIU hayana tofauti na matibabu kwa watu wengine, japo kuna muingiliano wa baadhi ya dawa za TB na dawa za kufubaza makali ya VVU (ART). Hivyo mtu anayeishi na maambukizi ya VVU na kukutwa na maambukizi ya TB anatakiwa kuanzishiwa dawa za TB kulingana na muongozo wa matibabu wa TB.

2.3.6 Matibabu ya Kifua Kikuu Sugu

Matibabu na muda wa matibabu ya TB sugu hutegemea aina ya usugu wa vimelea vya TB kwenye dawa zinazotumika kutibu TB. Mgonjwa anayetumia dawa za TB sugu, kila mwezi na pale inapohitajika anatakiwa kwenda katika kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi wa makohozi na vipimo vingine vya kimaabara na ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na umezaji wa dawa. Muda wa matibabu ya TB sugu ni miezi 9 hadi 24.

2.3.7 Matibabu ya Ukoma.

Matibabu ya ukoma yanategemea aina ya ukoma na umri wa mgonjwa. Mgonjwa wa ukoma humeza mseto wa dawa tatu.

Muda wa matibabu:

- Ukoma hafifu (PB) = miezi 6 mpaka 9
- Ukoma mkali (MB) = miezi 12 mpaka 18

Mgonjwa hupewa dawa za mwezi mmoja mmoja kumeza akiwa nyumbani. Mgonjwa humeza kidonge kimoja cha kwanza kila mwezi akiwa chini ya uangalizi wa mtoa huduma za afya wa kituo (DOT). Kila mwezi mgonjwa atatakiwa kufuata dawa na kwenda kituoni kwa ajili ya uchunguzi wa matumizi na madhara ya dawa.

2.3.8 Njia za Kujikinga Dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma

Kwa kiasi kikubwa, wagonjwa wenye ukoma mkali au TB ya mapafu ndio wanaoweza kuambukiza watu wengine kwa njia ya hewa. Msisitizo unawekwa kwenye kugundua mapema watu wenye kuugua magonjwa hayo. Hivyo ni muhimu kutoa elimu juu ya dalili za TB na ukoma kwa familia na jamii nzima ili wahisiwa wote waibuliwe mapema, kufanyiwa uchunguzi na kuwekwa kwenye matibabu ili kuzuia maambukizi ya TB na ukoma. Kuna njia tatu za kuzuia kuenea kwa TB ambazo ni:

Kuwa na Muundo na Mpangilio Rafiki wa Maeneo ya Kuishi na Utoaji Huduma.

Njia hizi uhusisha kupunguza hatari ya maambukizo (exposure) kama ifuatavyo:

- Kuwatambua mapema wote wenye dalili za TB na ukoma na kuwapa rufaa

- Kuhakikisha wote waliogundulika kuwa na TB au ukoma wanaanza matibabu mapema iwezekanavyo.
- Ufuatiliaji wa watu wanaoishi na wagonjwa wa TB na ukoma na kuwafanyia uchunguzi, pia kutoa rufaa kwa watoto chini ya miaka mitano.
- Kuelimisha wagonjwa wa TB na ukoma kuzingatia ufuasi mzuri wa dawa, kupima VVU na kuwatia moyo.
- Wagonjwa na familia zilizoathirika na jamii kwa ujumla kupewa taarifa zote muhimu na elimu kuhusu ugonjwa, matibabu na namna ya kujikinga.
- Utoaji wa chanjo (BCG) ya TB kwa watoto wote mara tu baada ya kuzaliwa.

• Wagonjwa wa TB na ukoma wasitengwe bali waanzishiwe matibabu mapema. Kwani, wakisha anza matibabu hawana uwezo wa kuambukiza watu wengine.

KUMBUKA



Kuboresha Mazingira ili Kuzuia Uwepo wa Vimelea.

Hizi ni njia zinazohusisha upunguzaji wa vimelea vya ugonjwa wa TB kwenye mazingira kwa kuhakikisha kuwa kuna mzunguko wa hewa ya kutosha na pia kupunguza msongamano kwa watu. Hii hujumuisha:

- Kuhakikisha nyumba zina madirisha makubwa yenye uwezo wa kupitisha hewa ya kutosha.
- Kuhakikisha madirisha na milango inafunguliwa mara kwa mara ili kuruhusu mzunguko wa hewa na mwanga wa kutosha.
- Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa, na tumia kiwiko cha mkono, kitaambaa au karatasi laini, fua kitambaa kwa maji na sabuni, osha mikono kwa maji tiririka na sabuni. Tupa karatasi laini iliyotumika kwenye ndoo yenye kifuniko.
- Kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Kujikinga Mtu Binafsi

Njia hizi hutumika pale ambapo njia za kimfumo na kimazingira haziwezi kupunguza uwezekano wa kuambukizwa vimelea vya TB kwenye jamii. Njia hizi ni pamoja na:

- Kula mlo kamili, kuepuka utapiamlo
- Kuepuka uvutaji wa sigara, matumizi ya dawa za kulevya, unywaji pombe uliopitiliza.
- Kupata matibabu haraka kuhusu hali yoyote ya kiafya.
- Kutumia vifaa vya kujikinga (mfano barakoa) unapokuwa katika mazingira yanayofikiriwa kuwa hatarishi kwa kuenea kwa magonjwa ya mfumo wa hewa (mfano maeneo ya migodini, misongamano ya watu, kambi za uvuvi na unapomtembelea mgonjwa wa TB sugu).

2.3.9 Namna ya Kutoa Huduma za Kifua Kikuu Majumbani na Kwenye Jamii Katika Kipindi cha Mlipuko wa Magonjwa Mbalimbali Ikiwemo UVIKO-19

Katika kipindi cha mlipuko wa magonjwa mbalimbali ikiwemo UVIKO-19(COVID-19), CHW unatakiwa kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Afya. Katika kipindi cha mlipuko wa magonjwa mbalimbali kama vile UVIKO-19, CHW unatakiwa kufanya yafuatayo:

- Kuvaa barakoa unapoenda kutoa huduma majumbani au kwenye jamii
- Kuepuka kumsogelea au kuwa karibu sana na mhisiwa wakati wa kutoa huduma
- Nawa mikono mara kwa mara kwa maji safi tiririka na sabuni kila baada ya kumhudumia mgonjwa.
- Kutumia vitakasa mikono (vipukusi/sanitaiza) pale inapohitajika
- Toa taarifa kwa mamlaka husika pale unapokutana na mgonjwa mwenye dalili za magonjwa mbalimbali ya mlipuko kama vile UVIKO-19
- Kula mlo kamili na toshelevu na kushiriki katika mazoezi mbalimbali ya mwili ili kujenga kinga ya mwili
- Kuepuka misongamano wakati wa kipindi cha mlipuko wa magonjwa

2.3.10 Tiba Kinga za Ugonjwa wa Kifua Kikuu

Hii huhusisha utoaji wa dawa kinga za TB kwa watoto walio chini ya miaka mitano wanaoishi na mgonjwa wa TB ambaye makohozi yake yamekutwa na vimelea vya TB. Dawa kinga za TB pia hutolewa kwa watu wote wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, ili kupunguza uwezekano wa kupata TB.

Kuzuia TB ni jukumu la wadau wote na jamii nzima na si jukumu la sekta ya afya pekee. Pia ni jukumu la kila mmoja katika kujikinga na magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya hewa ikiwemo TB na UVIKO-19 kwa kuzingatia kanuni za afya na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

KUMBUKA



SURA YA TATU

Utekelezaji wa Hatua za Udhibiti wa Kifua Kikuu, Ukoma Na Magonjwa Mseto Katika Ngazi ya Jamii.

3.1 Utangulizi

Huduma za TB na ukoma katika jamii ni sehemu ya jitihada za kugatua huduma za TB na ukoma toka vituo vya afya hadi kwenye jamii. Huduma hizi si mbadala wa vituo vya afya bali ni sehemu ya mkakati wa afya ya msingi ambao hushirikisha jamii ili kurahisisha huduma kwa wagonjwa na familia. Ingawa huduma za TB na ukoma zimeenea nchi nzima na kuleta matokeo mazuri ya matibabu ya TB na ukoma, bado kuna changamoto kadhaa katika udhibiti wa TB na ukoma nchini. Changamoto hizi ni pamoja na:

- Ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa wa TB, ukoma na magonjwa mseto ya TB
- Wagonjwa wa TB na ukoma kuchelewa kupata huduma za uchunguzi na matibabu mara wanapokuwa na dalili
- Ushiriki hafifu wa jamii katika kudhibiti TB na ukoma
- Unyanyapaa uliopo katika magonjwa ya TB na ukoma na UKIMWI
- Ufuasi hafifu wa matibabu ya TB ambayo huongeza tishio la usugu wa dawa

Kukabiliana na changamoto hizi, Wizara ya Afya, kupitia NTLP kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilianzisha mkakati wa kushirikisha jamii na vikundi vya watu waliowahi kuugua TB katika utoaji wa huduma za TB na ukoma. Hii itaboresha na kuhamasisha utafutaji na ufuatiliaji wa tiba, kuongeza ufahamu wa jamii kuhusu ugonjwa wa TB na ukoma, magonjwa mseto ya TB na kuzuia unyanyapaa. Udhibiti wa TB na ukoma katika jamii hujumuisha kazi mbalimbali katika jamii ambazo hufanywa na wanajamii wenyewe kwa kushirikiana na watoa uduma za afya ngazi ya jamii ambao ndio kiungo katika mfumo wa afya.

Watoa huduma za afya ngazi ya jamii wamepewa mafunzo maalum kuhusu kuzuia TB na ukoma, utambuzi wa mapema, jinsi ya kumhudumia na kumsimamia mgonjwa wa TB. Matokeo ya kushirikisha jamii katika huduma za udhibiti wa TB, ukoma na magonjwa mengine yanayohusiana nayo katika ngazi ya jamii yanalenga mambo yafuatayo:

- Wanajamii kujengewa uwezo wa kudhibiti tatizo la TB na ukoma.
- Kupunguza msongamano katika vituo vya tiba na hivyo kupunguza wingi wa kazi kwa watoa huduma za afya wachache waliopo.
- Kuongeza ufuasi wa matibabu ili kupunguza uwezekano wa kutokea kwa TB sugu
- Kupunguza maambukizi na vifo vitokanavyo na TB na ukoma.

3.2 Kazi za Udhibiti wa Kifua Kikuu, Ukoma na Magonjwa Mseto ya Kifua Kikuu Katika Jamii

Kazi za udhibiti wa TB na ukoma katika jamii zinahusisha shunguli mbalimbali zinazolenga kuleta matokeo chanya katika uzuiaji, ugunduzi, matibabu na matokeo mazuri ya tiba ya TB na ukoma. Kazi hizi ni pamoja na uhamasishaji wa jamii unaolenga kuleta mawasiliano na ushiriki miongoni mwa wanajamii. Kwa pamoja shughuli hizi zitaongeza mahitaji ya huduma za kinga, ugunduzi, matibabu na matunzo. Zifuatazo ni shughuli za udhibiti wa TB na ukoma katika jamii kwa kuzingatia matokeo yanayotarajiwa:

3.2.1 Kuongeza Ugunduzi wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma:

Kujenga Ufahamu

Kujenga ufahamu kuhusu udhibiti wa TB na ukoma utasaidia kuwafikia watu wenye uhitaji wa huduma hizo. Njia zifuatazo zitumeke katika kujenga ufahamu:

- Tembelea nyumba kwa nyumba ikiwa ni pamoja na jamii na familia zenye mazingira magumu.
- Shiriki kwenye mikutano mbalimbali ya kijamii na matukio maalum katika ngazi ya kijiji na kata

- Sambaza vifaa mbalimbali vya kuelimisha na mawasiliano.
- Toa shuhuda mbalimbali zinazohusu utokomezaji wa TB na ukoma
- Toa elimu ya afya katika vituo vya kutolea huduma za afya, makundi yaliyo katika hatari na jamii kwa ujumla



Picha na 3.1. Wanakikundi wa klabu ya waliowahi kuugua TB na ukoma wakihamasisha udhibiti wa TB na ukoma katika wilaya ya Temeke



Picha no 3.2: Mtoa huduma wa afya ngazi ya jamii akihamasisha wanajamii katika Manispaa ya Temeke.

Uhamasishaji katika Ngazi ya Kijiji/mtaa na Kata

Elezea taarifa za TB na ukoma katika mikutano ya kijiji/mtaa/kata na mikutano mingine ya hadhara kwa ajili ya kupata ushirikiano

Utafutaji wa Wenye Dalili za Kifua Kikuu au Ukoma Katika Jamii

Tembelea nyumba kwa nyumba:

- Tambua (uliza) wanakaya wenye dalili za TB na/au ukoma
- Orodhesha wanakaya wote waliofanyiwa uchunguzi wa awali wa TB/Ukoma katika fomu husika (TB/LEP 12)
- Toa rufaa kwa wale wote wanaohisiwa kuwa na TB au ukoma (TB/LEP 15)
- Andikisha wale wote wanaohisiwa kuwa na TB au ukoma kwenye rejesta ya wahisiwa wa TB na ukoma ngazi ya jamii (TB/LEP 13A)
- Fuatilia majibu ya makohozi na boresha rejesta ya TB na ukoma ya ngazi ya jamii
- Hakikisha wale wote waliothibitishwa kuwa na TB au ukoma wanaanza tiba mara tu wanapogulika.

Ufuatiliaji wa Watu Wanaoishi na Wagonjwa wa Kifua Kikuu au Ukoma Katika Kaya au Maeneo Mengine Wanapokaa

- Pata orodha na taarifa za watu waliothibitishwa kuwa na TB au ukoma kutoka kwa watoa huduma katika kliniki za TB na ukoma.
- Kwa kutumia wale waliothibitishwa kuwa na TB au ukoma, watambue wanakaya.
- Orodhesha wanakaya wote katika fomu husika (TB/LEP 12) na kuwafanyia uchunguzi.
- Toa rufaa kwa wale wote wanaohisiwa kuwa na TB au ukoma (TB/LEP 15). Andikisha wale wote wanaohisiwa kuwa na TB au ukoma kwenye rejesta ya TB na ukoma ya ngazi ya jamii (TB/LEP 13A).
- Fuatilia majibu ya makohozi na boresha rejesta ya TB na ukoma ya ngazi jamii (TB/LEP 13A).

- Hakikisha wale wote waliothibitishwa kuwa na TB au ukoma wanaanza tiba mara tu wanapothibitika

Ufuatiliaji wa Waliokatisha na Ambao Hawajaanza Matibabu

- Pata orodha na taarifa ya wagonjwa waliokatisha na ambao hawajaanza matibabu kutoka kwa watoa huduma katika kliniki za TB na ukoma.
- Fuatilia mara moja na toa mrejesho (tumia fomu ya kufuatilia waliokatisha na ambao hawajaanza matibabu) (TB/LEP 13B)

Ukusanyaji wa Sampuli za Makohozi

- Hakikisha mhisiwa wa TB anatoa sampuli yenye ubora.
- Zingatia hatua zote za usalama wakati wa kutoa sampuli.
- Kabidhi sampuli za makohozi katika kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu katika muda ulioelekezwa.

Sampuli za makohozi zikusanywe kwa wale tu wasioweza kufika katika kituo cha kutolea huduma za afya.

ANGALIZO



3.2.2 Kuboresha Matokeo ya Matibabu

Usaidizi wa Ufuasi wa Matibabu ya TB

- Toa usimamizi kwa mgonjwa wa TB ambaye anapata DOT nyumbani endapo umechaguliwa na mgonjwa. Pia fuatilia maendeleo ya wagonjwa wa TB na ukoma katika eneo lako.
- Wezesha kuanzishwa kwa vikundi vya uhamasishaji na ufuatiliaji wa matibabu
- Mfahamishe mgonjwa wa TB umuhimu wa ufuasi mzuri wa matibabu
- Ikumbushe familia kuhusu umuhimu wa ufuasi na utii wa kanuni za matibabu kwa mgonjwa wa TB
- Mfahamishe mgonjwa wa TB, familia yake na jamii kuhusu madhara ya ufuasi hafifu na kutokutii kanuni za matibabu ikiwemo TB

- Washirikishe viongozi wa jamii na watu mashuhuri endapo kuna changamoto



Picha no. 3.3: Mhudumu wa afya wa jamii akimsimamia mgonjwa wa TB na ukoma chini ya matibabu ya DOT nyumbani

Utunzaji na Utegemezi (Care and Support) kwa Mgonjwa wa TB na Ukoma, Familia na Jamii.

- Toa ushauri kuhusu lische ili kuzuia utapiamlo na kudhibiti magonjwa mengine
- Mtie moyo mgonjwa wa TB au UKOMA, familia na jamii
- Toa rufaa kwa mgonjwa mwenye changamoto inayohusu jinsia au haki za binadamu ambayo inaathiri huduma kwa mgonjwa kuendana na miongozo.

Kuboresha Udhibiti wa Maambukizi wa Kifua Kikuu na Ukoma

- Hakikisha unajikinga
 - Kuwa mwangalifu na upande unaokaa wakati wa mahojiano na mwenye dalili za TB au ukoma
 - Chukua tahadhari zote zilizoelekezwa ili kujikinga na maambukizo ya TB na ukoma

Udhibiti wa maambukizo ya TB na Ukoma

- Elimisha namna bora ya kukohoa kwa mgonjwa, familia na jamii kama ilivyoelekezwa katika miongozo



Picha no. 3.4. Ustaarabu wakati wa kukohoa ni njia mojawapo ya kuzuia maambukizo

- Elimisha umuhimu wa mzunguko mzuri wa hewa
- Hakikisha kila mtu aliyethibitishwa kuwa na TB au UKOMA anaanza tiba mara moja
- Mwelekeze mgonjwa wa TB kuwa makini wakati wa kutoa makohozi

Utoaji wa Huduma za Kifua Kikuu, Ukoma Katika Kipindi cha Mlipuko Katika Kipindi cha UVIKO-19

- Chukua tahadhari zote za kujikinga na maambukizi
- Toa elimu kuhusu kujikinga na maambukizi kwa mgonjwa na jamii
- Fuata taratibu na miongozo iliowekwa kuhusu UVIKO-19

Utoaji wa Huduma za Kifua Kikuu na Magonjwa Mseto ya Kifua Kikuu

TB na VVU, kisukari, utapiamlo na silikosisi

- Toa elimu kwa jamii juu ya magonjwa mseto ya TB kuendana na miongozo
- Tambua wenye dalili za magonjwa husika
- Toa rufaa kulingana na dalili za ugonjwa/magonjwa husika
